



Mmpango wa Ruzuku za Pembejeo za Kilimo unalenga kupunguza gharama za uzalishaji kwa mkulima mdogo au yule wa kujikimu. Sababu za mpango huu kama ulivyoelezwa kwenye sera za serikali ni pamoja na:

- ▶ kuongeza vipato kwa watu masikini;
- ▶ kupunguza gharama za vyakula;
- ▶ kuongeza uhakika wa chakula;
- ▶ kuhamasisha matumizi ya pembejeo za Mapinduzi ya Kijani;
- ▶ kuboresha ustawi wa wakulima;
- ▶ kuongeza rutuba ya udongo na;
- ▶ kutoa faida za kiuchumi kwa wakulima.

Ruzuku zinawalenga makundi maalum ya watu wajulikanao kama 'wanufaika'.

Ikiwa mkulima A anampatia mkulima B pakiti ya mbegu, mkulima B anakuwa amepata manufaa – hivyo mkulima B ni mnufaika.

Kwa kawaida, watu wanaopokea vifurushi vya mpango wa ruzuku ya pembejeo za kilimo (wanufaika) ni wale wakulima wa kujikimu.

Malengo ya Mpango wa Ruzuku za Pembejeo za Kilimo ni yapi?

Mpango wa ruzuku ya pembejeo za kilimo unagharimu kati ya dola za kimarekani milioni 100 na 160 kwa mwaka. Kwa kawaida, fedha hizi hutoka kwenye serikali za nchi na mifuko ya maendeleo.